Toleo la saba

Oktoba—Desemba 2007

Banana Investments Limited

Mbiu ya Banana

YALIYOMO

SALAAM ZA MKURUGENZI	**2**
	2
	3
CHUPA MPYA ZA KIOO ZENYE UJAZO 330 ML KUANZA KUTUMIKA ARUSHA	**4**
	4
CHUPA MPYA ZA PLASTIKI KUANZA KUTUMIKA KANDA YA ZIWA	**4**

BODI YA WAHARIRI

Augustine S. Mnja—Mwenyekiti

Michael D. Bessa– Katibu

Adolf R. Olomi—Mjumbe

Alphonsina A. Olomi– Mjumbe

Ibrahim Shigela– Mjumbe

Adolf N. May– Mjumbe

MAWASILIANO : *Banana Investments Limited*

Makao Makuu: Oloirien Village, SLP 10123 ARUSHA, Simu 0272506475, 0754224440, 0754888470. Fax 0272501549. Email banana@bol.co.tz

Dar es Salaam Depot: Manzese, kati ya Moshi Hotel na Lambo Bar, SLP 79407 Dar es Salaam, Simu 0222774276, 0746707983, 0784774148.

Rombo Depot: Tarakea, SLP 105 Tarakea, Simu 0787074436.

Tanga Depot: Barabara ya 4, karibu na Msikiti wa Vohora, SLP 5150 Tanga, Simu 0272646134.

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.7, JOktobai—Desemba 2007

MAONESHO YA BIASHARA YA PILI AFRIKA MASHARIKI – MWANZA.

Kampuni yetu ilishiriki maonesho ya pili ya kibiashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika katika viwanja vya Sabasaba Ilemela Mwanza kuanzia tarehe 31 August- 10 September 2007.Maonesho haya ambayo yaliandaliwa na chama cha wenye viwanda, biashara na kilimo Mkoa wamwanza (TCCIA) yalishirikisha makampuni ya kibiashara na huduma toka Tanzania,Kenya,Uganda na Zimbabwe.Kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa ni ***"Kuzileta nchi za Afrika Mashariki Karibu"***

Maonesho haya yalifunguliwa rasimi na Waziri wa mambo ya nje na ushirikiano wa Kimataifa Mh. Bernard Membe tarehe 5/9/2007 ambapo pia alitoa zawadi mbalimbali na vyeti kwa washindi katika makundi mbalimbali.

Katika maonesho haya,banda la kampuni yetu liliwavutia watu wengi sana kwa kuona bidhaa zetu zenye kukidhi ubora na haja ya mlaji kwa bei nafuu.Pia tulikuwa na video ambayo ilionesha hatua mbalimbali za uzalishaji kiwandani hadi kwenye soko.Watu wengi waliofika kwenye banda letu wlivutiwa sana nakuweza kutofautisha bidhaa zetu na zile za makampuni mengine ya usindikaji.Miongoni mwa watu waliotembelea banda letu ni pamoja na maofisa wa Mamlaka ya Vyakula na Madawa mkoa wa Mwanza ambao pia walivutiwa sana na ufungaji mpya wa kinywaji cha Raha kwenye chupa ya Plastiki (PET).

Pia kuna wafanya biashara wapatao tisa kutoka kanda ya Ziwa na Kenya ambao wamejitokeza kutaka kufanya biashara na sisi .Kati yao wanne tayari wameshaleta maombi yao rasmi nakukubaliwa baada ya kutimiza masharti ya uwakala .Soko hili ni kubwa sana hivyo bado kuna nafasi ya kuongeza wakala wengine na tunakaribisha maombi mapya

Imeandaliwa na ***Adolf N Mlay***
Meneja Masoko.

SOKO LA KANDA YA ZIWA LIMEANZA TENA

Itakumbukwa kwamba tulisitisha kutoa huduma kwa soko la kanda ya Ziwa tangu mwezi May mwaka jana kutokana na sababu za kiufundi.Baada ya kujipanga upya tumeanza kutoa huduma kama kawaida.Kwa mara hii tunatumia chupa za plastiki (PET) ambazo zimetengenezwa kitaalam na kuhakikiwa na mamlaka ya vyakula na madawa pamoja na shirika la viwango Tanzania (TBS).

Kwa wauzaji wa Mwanza watapata bidhaa zetu kwa Life General Stores duka lililopo mtaa wa Liberty na kwa A.A Tarimo pia wa mtaa huohuo. Kwa wakazi wa Shinyanga watapata huduma hiyo kwenye duka la Bw.Minja karibu na soko kuu la Shinyanga .Pia wapo Mjini Kahama.

Tunayo matarajio ya kuwapata wateja wengi zaidi maeneo Nzega,Tabora Mjini na Musoma . Lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunawafikia wateja wote wa Kanda hii ifikapo mwaka 2009.

Imeandaliwa ***A.A Mlay***
Meneja Masoko.

Mbiu ya Banana

Jarida lizilewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.7, JOktobai—Desemba 2007

AJIRA MPYA KAMPUNI YA BANANA

Pamoja waajiriwa watano waliotajwa katika toleo lililopita, mwaka huu hadi Julai kampuni imeajiri katika idara mbalimbali kama ifuatavyo:

James E. Lyimo – Mhasibu Msaidizi

Bwana Lyimo ana Stashahada ya Uhasibu na uzoefu wa mwaka mmoja katika fani hiyo.

Venosa Sabas – Afisa Manunuzi

Bi Venosa Sabas ana Stashahada ya Ugavi (Materials Management) na uzoefu wa mwaka mmoja katika fani hiyo.

Jeyaprakash Kunjupillai – Meneja Uzalishaji Mwandamizi.

vana Kunjupillai ana Shahada ya .andisi na uzoefu kazini wa miaka 14 tika viwanda mbalimbali vya kuten-neza vinywaji.

Azza Mrinji. – Dereva Mauzo

Azza Mrinji ana Shahada Biashara na Usimamizi wa Masoko ya Chuo cha Nairobi, na Cheti cha mauzo – Dar-es-Salaam. Ana uzoefu wa miaka 12 (kumi na mbili) katika fani hiyo.

John Mgonja. – Dereva Mauzo

John Mgonja ana vyeti vya udereva kutoka VETA, utengenezaji wa magari na VTC. Anao uzoefu wa miaka sita (6) katika kuendesha magari makubwa na madogo.

Patrick S. Mushi – Afisa Utawala

Bwana Mushi ana Stashahada ya Rasilimali-watu na uzoefu wa mwaka mmoja katika fani hiyo.

Hashimu Adam. – Fundi wa kuosha Magari.

Hashimu Adam ana Leseni ya Udereva toka KIBO DRIVING SCHOOL – ARUSHA. Ana uzoefu wa kuendesha na kuosha magari kwa miaka miwili.

Martine K. Msofe. – Mlinzi

Martine Msofe ana Cheti cha Theology na Philosophy na ni mkufunzi wa Ulinzi. Ana uzoefu wa miaka 16 katika fani ya ulinzi.

Stephen J. Swai. – Dereva Mauzo.

Stephen Swai ana Leseni ya Udereva toka VETA (Vocation Education and Training Authority) – Moshi. na uzoefu wa miaka mitatu katika fani hiyo.

Witness Nkini. – Mlinzi.

Witness Nkini ana Cheti cha Ma-funzo ya Ulinzi toka katika kituo cha mafunzo cha Watch & Guard (T) Ltd Training School. Ana uzoefu wa mi-aka saba katika fani hiyo.

Abubakar Munishi. – Dereva Mauzo

Abubakar ana Cheti cha Udereva na uzoefu wa kuendesha magari ya aina zote (makubwa na madogo). Pia nao uzoefu wa miaka kumi ya uuzaji na usambazaji wa bidhaa mbalimbali.

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.7, JOktobai—Desemba 2007

CHUPA MPYA ZA KIOO ZENYE UJAZO 330 ML KUANZA KUTUMIKA ARUSHA

Kuendana na maendeleo ya kuboresha uzalishaji, kampuni imenunua mashine za kisasa za kusafisha na kujaza mvinyo kwenye chupa. Mashine hizo zitatumia chupa maalum za kioo zenye nembo ya kampuni.

Chupa hizo ni imara na thabiti na zinaweza kuingia katika mzunguko wa soko mara kumi au zaidi. Kutokana na muundo na ubora wake, chupa hizo zimenunuliwa kwa bei kubwa, jambo ambalo limelazimisha dipositi kwa ajili ya chupa hizo kuongezeka.

Chupa mpya zitawafikia wateja kwa kutumia kreti za plastiki ambazo tayari ziko sokoni, hivyo dipositi kwa ajili ya kreti haitabadilika.

Kwa kuanzia chupa mpya zitaanza kutumika kusambaza bidhaa zetu Mkoa wa Arusha na baadaye kuenezwa katika mikoa mingine ya Tanzania.

Imeandikwa na
Augustine S. Minja

CHUPA MPYA ZA PLASTIKI KUANZA KUTUMIKA KANDA YA ZIWA

Katika toleo lililopita jarida hili lilidokeza wazo la kampuni kuanza kuuza bidhaa zake ndani ya chupa za plastiki (PET Bottles) za ujazo wa 330 ml. Chupa hizo hutumika mara moja na hazitahitaji kuwa kwenye mzunguko kama zilivyo chupa za kioo. Chupa hizi zitawafikia wateja ndani ya katoni za chupa 12 ambazo zimeshazoeleka.

Hii ni hatua nyingine ya kuboresha huduma kwa wateja wetu kwani, wateja hawataingia gharama za dipositi kwa ajili ya kreti na chupa tupu. Baada ya kuanza kutolewa kwa huduma hii bidhaa zetu zitawafikia wateja katika maeneo ya mbali na ya karibu na kiwanda, na wasambazaji hawataingia katika usumbufu wa kurejesha matupu (kreti na chupa) kiwandani.

Zikiwa zimefungwa ndani ya chupa za plastiki, bidhaa zetu zitaweza kuuzika kiurahisi kwenye mabaa na madukani, hivyo kuwafikia walengwa kwa urahisi zaidi.

Imeandikwa na
Augustine S. Minja